# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

## CHUO CHA UFUNDI ARUSHA

# TAARIFA KWA UMMA

## KUFUNGULIWA KWA CHUO KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026

Arusha, Novemba13, 2025

Mkuu wa Chuo cha Ufundi Arusha (ATC) anapenda kuwatangazia wanafunzi wote kuwa, Chuo kitafunguliwa tarehe 17 Novemba, 2025 siku ya Jumatatu kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza na Kwa Wanafunzi Wanaoendelea na masomo tarehe 24 Novemba, 2025.

**Mambo ya kuzingatia wakati wa kuripoti Chuoni:**

**Wanafunzi wa mwaka wa kwanza:**

1. Kuhakikisha kuwa umechaguliwa kujiunga na chuo cha Ufundi Arusha

2. Kuhakikisha kuwa una joining instructions (maelekezo ya kujiunga), fomu ya hospitali, vyeti halisi na nakala za vyeti vya shule (kidato cha nne, sita na diploma) na kuzaliwa

3. Hakikisha umelipa ada yote ya muhula wa kwanza na michango mingine (Direct cost)

4. Utaratibu wa usajili ufuatwe kulingana na tangazo la usajili mara ufikapo chuoni

5. Kwa mwenye Bima ya AFYA NHIF afike nayo na nakala yake ili uhakiki ufanyike

6.kuhudhuria ***orientation*** kulingana na ratiba pendekezwa.

**Kwa Wanachuo Wanaoendelea na Masomo:**

1. Usajili utafanyika kama unavyofanyika kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza zingatia muda wa kuripoti na usiingie darasani mpaka ukamilishe usajili.

2. Hakikisha umelipa ada yote ya muhula wa kwanza na michango mingine (Direct cost)

Kwa wanachuo wote usajili utafanyika kwenye tovuti ya chuo www.atc.ac.tz kwa wale watakaoshindwa kutakuwa na Dawati la usaidizi mara wafikapo chuoni.

Chuo kinatoa wito kwa Wanachuo wote kuzingatia tarehe ya kufungua chuo na tarehe ya mwisho ya Usajili ambayo ni tarehe 01 Desemba 2025 kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza na wanachuo wanaoendelea na masomo ni tarehe 08 Desemba, 2025 Kwa atakayechelewa baada ya tarehe hiyo atakuwa amepoteza nafasi yake.

Wote mnakaribishwa.

Kwa maelezo zaidi wasilina nasi: +255734 602 000/+255 734 800 500

Imetolewa na;

kitengo cha Mawasiliano na masoko-Chuo cha Ufundi Arusha